

# JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Kumb. Na.DCC/AC.66/1

Tarehe 24/04/2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam amepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa Fedha 2022/2023 yenye Kumb. Na. FA.97/228/01'TEMP'/06 ya tarehe 06 Aprili, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo Mkurugenzi wa Jiji Dar es Salaam anawatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi ziliyotajwa hapa chini kama ifuatavyo:-

### 1. MTENDAJI WA MTAA DARAJA III : NAFASI 5

#### SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Awe na Elimu kuanzia Kidato cha Nne/Sita
- ii. Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada (cheti) NTA Level 5 kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali katika fani zifuatazo:
  - Utawala
  - Sheria
  - Elimu ya Jamii
  - Usimamizi wa Fedha
  - Maendeleo ya Jamii
  - Sayansi ya Jamii

## **KAZI NA MAJUKUMU:**

- Katibu wa Kamati ya Mtaa
- Mtendaji Mkuu wa Mtaa
- Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu Mipango ya Maendeleo katika Mtaa
- Msimamizi wa Utekelezaji Sheria ndogo pamoja na Sheria nyingine zinazotumika katika Mtaa
- Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama
- Msimamizi wa Utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa
- Kusimamia ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa Kodi wote katika Mtaa
- Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

## **MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara wa Serikali yaani TGS B kwa mwezi

## **2. MASHARTI KWA UJUMLA**

- Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka kumi na nane (18) na usiozidi miaka arobaini na tano (45)
- Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
- Mwombaji aambatishe Cheti cha Taaluma, Cheti cha Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) pamoja na picha moja ya rangi (passport size)
- Waombaji ambao wamesoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE

- Testmonial, Provisional Results, Statement of Results, Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita HAVITAKUBALIWA
- Uwasilishaji wa taarifa za sifa za kughushi ni kosa la jinai hivyo wahusika watachukuliwa hatua za kisheria
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 3/5/2023 saa 9.30 alasiri.

***Jinsi ya kutuma maombi:***

Barua zote za maombi ya kazi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili na namba za simu za mwombaji, Barua Pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa anwani ufuatayo:-

*Mkurugenzi wa Jiji,*

*Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,*


*1Mtaa wa Mission*

*S.L.P 20950,*

**DAR ES SALAAM**

**AIDHA, TANGANZO HILI LINAFAUTA TANGAZO LA TAREHE 19/04/2023 AMBALO LILIKOSEWA TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI.**

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:**



Eng. Amani I.B. Mafuru

**KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**